Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili - 00005809 Toleo 16: Desemba, 2014

Huduma bora za afya kwa watanzania wote

Mkurugenzi Mtendaji wa Sikika Bw. Irenei Kiria (Kushoto) akisalimiana na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Dk. Seif Rashid pamoja na Naibu wake Dk. Steven Kebwe nje ya ukumbi wa mikutano wa Kunduchi Beach Resort, jijini Dar es salaam walipohudhuria mkutano wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now 2014).

Utangulizi

TOLEO hili la 16 linaelezea kwa ufupi baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na shirika katika robo ya nne ya mwaka huu (2014).

Katika kipindi hiki cha robo ya mwisho ya mwaka, Sikika iliendelea kutekeleza kwa mafanikio shughuli za Ufuatiliaji Uwajibikaji kwa Jamii (Social Accountability Monitoring-SAM) katika wilaya za SingidaVijijini, Mpwapwa na Kondoa (Dodoma).

Katika wilaya hizo, Sikika ilibaini changamoto mbalimbali zikiwemo upungufu wa dawa katika baadhi ya vituo vya afya, uchakavu wa majengo, mapungufu katika ujenzi wa vizimba vya kutupa taka mbichi na mgawanyo usio sawia wa watumishi kwenye maeneo ya pembezoni. Hata hivyo, baadhi ya madiwani kwa kushirikiana na halmashauri walianza kuzifanyia kazi changamoto hizo.

Aidha, Sikika pia ilipata fursa ya kushiriki katika mkutano wa wadau wa uandaaji wa malengo ya kitaifa ya mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN), kwenye sekta ya afya ambapo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilipitisha malengo makuu manne yanayoanza kutekelezwa mwaka 2015.

Kwa taarifa zaidi kuhusu kazi za Sikika, tafadhali peruzi tovuti yetu; *www.sikika.or.tz*, twitter - *@sikika1*, facebook - *Sikika Tanzania* na blogspot - *www.sikika-tz.blogspot.com.* Kwa maoni tafadhali wasiliana nasi kupitia *info@sikika.or.tz* au sms *0688-493-882*.

Karibu!

NDANI

Sikika yapendekeza vipaumbele vya afya BRN.....2
Simanjiro waendelea kutekeleza maazimio ya SAM 2
Upungufu wa Dawa waiathiri Mpwapwa 3
Mgawanyo watumishi uzingatie maeneo ya pembezoni 4

Sikika yapendekeza vipaumbele vya afya BRN

Na Beatrice Mkani

Katika robo ya mwisho wa mwaka (2014), Sikika ilipata fursa ya kushiriki katika mkutano wa wadau wa uandaaji wa malengo ya kitaifa ya mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN), kwenye sekta ya afya.

Awali, mpango huo haukuwa umeanisha sekta ya afya kama moja ya maeneo ya kipaumbele hadi mwaka huu (2014) ambapo sekta ya afya nayo iliingizwa. Utekelezaji wa BRN katika sekta ya afya utaanza 2015 hadi mwaka 2017 kwa kuanza na mikoa michache na kisha kupanuka kufikia maeneo mengine ya nchini. Lengo kuu ni kuharakisha na kuboresha utoaji na upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Mchango wa Sikika, kwanza, ulisisitiza kuboresha maeneo yanayohusu uwajibikaji na uwazi kwenye utawala na usimamizi wa fedha za afya ili wananchi wengi waweze kupata huduma bora. Hii ni pamoja na kuimarisha mifumo ya bima za afya zenye lengo la kupanua wigo wa wananchi kufikiwa na huduma hizo muhimu.

Pili, Sikika ilisisitiza umuhimu wa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na kufanyiwa kazi kwa changamoto sugu za upungufu wa dawa na vifaa tiba muhimu katika vituo vya afya vya umma na zahanati.

Mchango wa tatu ulijikita katika kutathmini Rasilimali watu katika sekta ya afya. Nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa wafanyakazi hususan maeneo ya vijijini. Upungufu huu unachangiwa na bajeti finyu na kukosekana kwa vivutio kwa wafanyakazi hasa wa maeneo yaliyoko pembezoni. Wafanyakazi wengi wa sekta ya afya wamekuwa wakikimbia maeneo ya vijijini kutokana na mazingira magumu ya kazi. Shirika lilisisitiza umuhimu wa BRN kuangalia suala hili.

Mwisho, Sikika ilipendekeza ushirikishaji wa wananchi katika kuandaa mipango na kupanga bajeti kwenye ngazi za serikali za Mtaa/Kijiji. Baadhi ya mifumo inayotumika kuandaa bajeti inabidi iboreshwe ili vipaumbele vya wananchi viweze kujumuishwa katika bajeti.

Baada ya kusikiliza maoni ya wadau, ikiwemo Sikika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilianisha malengo makuu manne yanayoanza kutekelezwa mwaka 2015. Malengo hayo ni; afya ya uzazi, vichanga na watoto – lengo ni kupunguza vifo vya akinamama, vichanga na watoto kwa 20%.

Mengine ni usambazaji wa rasilimali watu katika sekta ya afya – kwa lengo la kuinua mikoa 9 ambayo inakabiliwa na tatizo sugu la upungufu wa wafayakazi na kuongeza upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba nchini kwa 100%. Lengo lingine ni kukuza ufanisi katika kutoa huduma kwenye ngazi ya vituo vya afya na zahanati.

BRN ni mfumo wa kisayansi wa maendeleo unaoweka vipaumbele, malengo na muda wa utekelezaji, ufuatiliaji makini wa uwajibikaji hadi kufikia matokeo yaliyopangwa.

Simanjiro waendelea kutekeleza maazimio ya SAM

Na Fredrick Ngao, Simanjiro

Baadhi ya wajumbe wa timu ya SAM wilayani Simanjiro wakipata ufafanuzi kutoka kwa Muuguzi wa zahanati moja wilayani humo.

Baraza la Madiwani wakishirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Simanjiro wameendelea kufanyia kazi changamoto zilizoibuliwa katika utekelezaji wa zoezi la SAM na hivyo kuanza kuleta mabadiliko katika utoaji wa huduma kwenye zahanati na vituo vya afya.

Awali, taasisi ya Sikika iliratibu mafunzo kwa timu ya SAM ya halmashari ya Simanjiro. Baada ya mafunzo hayo, timu hiyo ilitembelea miradi ya maendeleo na kuibua changamoto kadhaa katika baadhi ya miradi. Mfano, yapo majengo yaliyoripotiwa kujengwa chini ya kiwango kama majengo ya kituo cha afya cha Kitwai, zahanati ya Engonongoi na msingi wa zahanati ya Losinyai.

Changamoto nyingine zilikuwa ni, ubovu wa tangi la kuhifadhia maji la Naberera ambalo tayari limeshakarabatiwa. Ujenzi wa shimo jipya la kutupa

taka mbichi katika kituo cha afya cha Naberera nao umekamilika. Vituo vilivyoripotiwa na timu ya SAM kuwa na upungufu wa watumishi kama Kimotorok, Orchoronyori, Magadini na Kitwai, navyo vimepata wahudumu wapya.

Timu pia iliripoti umuhimu wa kudhibiti upotevu wa dawa vituoni jambo ambalo Mganga Mkuu wa Wilaya ameanza kulifanyia kazi na matokeo yameanza kuonekana. Vilevile madiwani wamekuwa wakihimiza watendaji wa kata kuhakikisha wananchi wanajiunga na mfuko wa afya ya jamii (CHF) na wengi wameanza kujiunga.

Yote hayo yamepata ufumbuzi kutokana na madiwani kutekeleza vyema jukumu lao la uwakilishi wa wananchi na usimamizi kwa watendaji wa Halmashauri, hali ambayo imechochea uwajibikaji wa watendaji. Madiwani wa wilaya hii wamethibitisha kuwa chombo cha uwakilishi wa wananchi na usimamizi wa halmashauri.

Katika kusisitiza uwazi na uwajibikaji, Mbunge wa Simanjiro Mh. Christopher Ole Sendeka aliwataka watendaji wote katika halmashauri hiyo kuwa makini na kutekeleza miradi yote ya maendeleo kwa uadilifu, kulingana na thamani ya fedha. Kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha Oktoba-2014, Mh. Ole Sendeka pia aliwasisitiza madiwani kusimamia kikamilifu fedha za umma ili kuwapatia wananchi huduma bora.

Upungufu wa Dawa waiathiri Mpwapwa

Na Richard Msittu, Mpwapwa

Kati ya Oktoba na Novemba, 2014 nchi ilikumbwa na upungufu mkubwa wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Upungufu huo kwa kiasi kikubwa ulisababishwa na Serikali kushindwa kulipa limbikizo la deni kwa shirika la ununuzi na usambazaji wa dawa (MSD), hivyo kusitisha utoaji huduma.

Kushindwa kusambaza dawa katika vituo mbalimbali nchini, pia kuliiathiri wilaya ya Mpwapwa na vitongoji vyake. Ufuatiliaji vituoni pia ulibaini kuwa kati ya vituo 34 vilivyotembelewa, vituo 31 vilikuwa na dawa pungufu ya mahitaji au havikuwa na dawa kabisa.Hata hivyo, dawa zinazosambazwa kwa ufadhili wa miradi msonge (Vertical Programs) kama za UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria zilikuwepo.

Wakati vituo vingi vikiwa na uhaba huo, vituo vichache vilionekana kuwa na wingi wa baadhi ya vifaa tiba, mfano, zahanati za Winza na Inzonvu zilizotembelewa na Sikika ziligundulika kukosa vifaa tiba kama glovu wakati zahanati ya Chunyu kulikuwa na glovu zenye thamani ya Shilingi 400,000/= ambazo ni mara 5 ya mahitaji halisi kwa zahanati hiyo, huku ikikosa dawa nyingine. Zahanati za Wangi na Mlunga zilizokuwa ndio kwanza zimefunguliwa baada ya kutelekezwa kwa muda mrefu pia zilikumbwa na ukosefu wa dawa.

Wananchi wenye vipato vya chini ndio waliokuwa wahanga wakubwa wa kadhia hii kwani walilazimika aidha kusubiri usambazaji wa mwezi Novemba ama kudra za watoa huduma ambao kimsingi hawakuwa na msaada. Wananchi wengine walilazimika kutafuta huduma katika vituo vya binafsi ambavyo ni vichache, ghali na vingi havikidhi huduma. Aidha, kadhia hiyo iliwaathiri zaidi wagonjwa waliokuwa wamelazwa vituoni ambao hawakuwa na njia mbadala zaidi ya kustahimili maumivu, Akinamama wajawazito na watoto ambao kwa asilimia kubwa ndio watumiaji wa huduma za afya nao hawakuwa salama.

Mratibu wa Sikika wilayani Mpwapwa Richard Msittu akiongea na wananchi katika moja ya kituo cha afya wilayani humo.

Ili kuweka msukumo wa kukabiliana na changamoto hii kitaifa, vyombo vya habari na baadhi ya asasi za kiraia, ikiwemo Sikika, zilitoa matamko ya kuitaka serikali kusambaza dawa kwa haraka. Mijadala ya Wabunge waliokuwa wakiendelea na vikao vya Bunge nayo ilihimiza serikali kuchukua hatua za haraka. Hatua hiyo ilipelekea Wizara za Fedha na Afya kutoa fedha kiasi zilizoiwezesha MSD kuanza kurejesha huduma taratibu

Pamoja na kuanza kurejea kwa huduma ya usambazaji wa dawa vituoni, bado kiwango cha usambazaji hakikidhi mahitaji halisi. Mfano, kwa upande wa mahitaji ya dawa kwa watoto chini ya miaka mitano, bado haijafikiwa..

Hata hivyo, Shirika linawapongeza madiwani kwa kutumia vema kikao cha Novemba 2014 kuagiza Halmashauri kuweka kipaumbele kwenye ununuzi wa dawa za watoto chini ya miaka 5 kupitia mfuko wa CHF. Ni imani yetu kuwa hatua hii itakuwa endelevu

na itasimamiwa kikamilifu ili hatimaye Wilaya iweze kufikia lengo la upatikanaji wa huduma bora za afya kwa Watanzania wote.

Sekta ya Afya nchini ni muhimu katika mustakabili wa Taifa kwani athari zake zinagusa moja kwa moja nguvukazi ya Taifa na maendeleo kwa ujumla. Kama sehemu ya kuboresha juhudi za upatikanaji dawa, tunaishauri halmashauri kuwekeza nguvu nyingi kwenye njia mbadala za kugharamia huduma za afya ikiwemo kupitia Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) na vyanzo vingine.

Mgawanyo watumishi uzingatie maeneo ya pembezoni

Na Ally Abdallah, Kiteto

Baadhi ya wananchi wakisubiri kupata huduma ya afya katika moja ya kituo cha afya wilayani Kiteto.

Tatizo la upungufu wa rasilimali watu kwenye sekta ya afya limetajwa kuwa kikwazo katika utoaji huduma za afya hasa katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwamo. Licha ya jitihada zinazofanyika na serikali kukabiliana na upungufu wa watumishi wa afya, hali bado hairidhishi hasa katika maeneo ya vijijini.

Sababu nyingi zimekuwa zikitajwa ikiwemo mazingira magumu ya kufanyia kazi, uhaba wa vitendea kazi pamoja na kukosekana kwa motisha kwa wafanyakazi wa vijijini. Hali hii imekuwa ikiwanyima wananchi wengi haki ya kupata huduma bora za afya ikizingatiwa kwamba wengi wana hali ngumu kiuchumi na wanategemea huduma kutoka katika vituo vya afya vya umma.

Moja ya shughuli za Sikika ni kufuatilia utoaji na upatikanaji wa huduma za afya katika baadhi ya vituo na hospitali za umma. Wilayani Kiteto, ufuatiliaji ulibaini upungufu pamoja na mgao usio sawia wa watumishi kwenye baadhi ya vituo. Maeneo yaliyoko mbali na mji hali ilikuwa mbaya. Mathalan, zahanati ya Ng'abolo ilikuwa na watumishi wawili tu ambapo mmoja ni mhudumu wa afya (Medical attendant) na mwingine ni Tabibu msaidizi (Clinical Assistant).

Katika zahanati ya Njoro, kwa mfano, kulibainika kuwa na wakunga (Nurse midwife) zaidi ya wawili wakati zahanati ya Ng'abolo haikuwa na mkunga hata mmoja. Hali hiyo imekuwa kero kwa wakazi wa Ng'abolo hasa akinamama ambao hulazimika kufuata huduma za mama na mtoto/kliniki umbali wa zaidi ya kilomita 15.

Ufuatiliaji pia uligundua kwamba upungufu wa watumishi unazikabili zahanati za Loltepes, Laiseri na Irkiushibor. Wananchi wa maeneo hayo wanapata shida kutokana na kukosekana kwa watumishi wa kutosha. Tunatoa rai kwa wananchi wa maeneo husika kuwajibika na kudai haki yao ya kupata huduma bora za afya kwa kufuatilia na kushiriki kikamilifu katika mikutano ya kupanga na kusimamia mipango ya afya.

Kwa kutambua ugumu wa mazingira ya maeneo hayo, tunaishauri halmashauri ya wilaya ya Kiteto kuwa na utaratibu wa kutoa motisha kwa watumishi wanaopangwa kufanya kazi kwenye vijiji/vitongoji hivyo, ikiwemo kuwapa nyenzo za usafiri kama pikipiki.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57

Ujumbe mfupi: 0688493882
Faksi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Faksi: 026 23 21316